
# Kuhami Uhuru Wetu:Kambi Za Kijeshi Za Marekani Katika Afrika na Mustakabali Wa Umoja Wa Afrika.

**Dozia no. 42  Chapisho la pamoja na kituo cha utafiti cha Vuguvugu la Wajamaa la Ghana(SMG)**




Baadhi ya kambi za kudumu na za muda mfupi zinazofahamika za Kamandi ya Afrika ya Jeshi la Marekani barani Afrika(AFRICOM),2019.

Unawezaje kuziona alama za nyayo za milki kubwa?

Taswira zilizomo katika dozia hii zinaonesha baadhi ya kambi za kijeshi za AFRICOM(kamandi ya bara la Afrika ya jeshi la Marekani) katika bara la Afrika-zote 'za kudumu ' na 'za muda mfupi',kama ziitwavyo kwa urasmi.Picha za satelaiti zilikusanywa kwa data na msanifu Josh Begley,ambaye aliongoza **mradi** wa kuainisha kwa kupiga picha na kuweka alama ili kujibu swali: 'unawaezaje kupima alama za nyayo za kijeshi?'

Kwa dozia hii, taasisi ya utafiti wa kijamii ya Tricontinental iliweka taswira na majira nukta ya maeneo hayo yaliyofichwa-kabisa katika ramani ya Afrika, na kuonesha hali ya leo ya kuongezeka kwa shughuli za kijeshi.

Wakati huohuo, pini na nyuzi zinazounganisha maeneo haya zinatukumbusha juu ya 'maeneo ya vita' ya mabavu ya ukoloni. Kwa pamoja, seti ya taswira ni ushahidi unaoonekana wa kuendelea 'kumegwa na kushurutishwa kwa watu na serikali za bara hili', kama dozia inavyoandika.



Tunakataa kusalia bila tija. Tunataka kupunguza mgandamizo dhidi yetu, kukomboa viijiji vyetu kutoka katika mkwamo ama mgandamizo wa muda mrefu.Tunataka kuifanya jamii yetu kuwa ya kidemokrasia, kufungua ufahamu wetu katika ulimwengu wa wajibu wa pamoja, ili tuweze kuwa madhubuti  na kuvumbua kesho yetu. Tunataka kubadili uongozi na kuu-unda kwa mtindo tofauti wa utumishi wa umma. Tunataka tulifanye jeshi letu lishiriki na watu katika uzalishaji na kulikumbusha wakati wote kuwa, bila mafunzo ya uzalendo mwanajeshi ni sawa na muhalifu mwenye mamlaka. Hiyo ndio programu yetu ya kisiasa.

Thomas Sankara (Rais, Burkina Faso) akiwa Umoja wa Mataifa, 4 Octoba 1984.

Mei 30,2016, Baraza la Usalama na Amani la Umoja wa Afrika(PSC) lilifanya kikao chake cha 601. Japokuwa agenda ulikuwa pana,wajumbe wa PCS walikuwa kikaoni wakiwa na wasiwasi juu ya migogoro kadha wa kadha:kuanguka kwa dola la Libya na madhara yake kwa ukanda wa Sahel, mapambano yaliyokuwa yakiendelea katika ukanda wa ziwa Chad ambako Boko Haram walikuwa wameendelea kukita mizizi. PSC haikuhitaji somo kutoka kwa yeyote juu ya udhaifu/ukomo wake ambao ulikuwa wa namna-mbili:

1. . Miezi michache kabla ya mkutano wa Mei, PSC **liliidhinisha** wanajeshi 5,000 wa Misheni ya Kukinga na Kuzuia ya Afrika(*African Prevention and Protection Mission*) kwenda nchini Burundi.Hii kwa sehemu ilitokana na migogoro isiyokwisha katika eneo la maziwa makuu,ambayo ilihusisha vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Burundi(1993-2005) vilivyoambatana na mgogoro wa kisiasa uliotokana na hatua za Rais Pierre Nkurunziza kuukaba mfumo wa kisiasa wa nchi hiyo,hali iliyopelekea machafuko na ukatili wa dola mwaka 2015. Rais Nkurunziza alifanya jitihada kupenyeza agenda miongoni mwa wakuu wa nchi za kiafrika kuzuia maamuzi ya PSC. AU ukaamua baadaye kuwa hali nchini Burundi ilikuwa imetengemaa, licha ya ushahidi wa Umoja wa Mataifa kuonesha uhalifu wa makosa dhidi ya binadamu. Hili lilikuwa mfano

mmojawapo unaoonesha kugawanyika kwa uongozi wa Afrika,ambao uliiizuia PSC kutekeleza agenda zake.

2. **Migandamizo kutoka nje**. Kati ya February na Machi 2011, PSC **lilikutana** kuunda mpango kazi kamili wa kutafuta suluhu ya mgogoro wa Libya. Ujumbe wa PSC **ulikutana** Nouakchott,Mauritania ili kusafiri kwenda Tripoli, Libya na kufungua mazungumzo ya kusaka amani kwa kadiri ya ibada ya 7 ya **itifak**i ya PSC. Aya ya ibara hii-ambayo ilikuwa ikifahamika kama 'mwongozo' - inahusisha njia za namna nne,ikiwamo kusitisha mapigano,kuruhusu misaada ya kibinadamu kwa ushirikiano,kulinda raia wa kigeni na kuchukua hatua ya mageuzi ya kisiasa katika kuondoa visababishi vya mgogoro. Serikali ya Libya na wapinzani wote **waliukataa** muongozo huu awali, ingawa nafasi ya mjadala iliendelea kuwepo,ndio sababu ujumbe wa PSC ulikuwa tayari kwenda Tripoli.Siku moja kabla ujumbe wa PSC haujaondoka ,Ufaransa na Marekani zilianza kuilipua kwa mabomu Libya. Ulipuaji ulifanyika chini ya kinga ya nchi za NATO na azimio namba 1973 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lililopigiwa kura na nchi tatu za kiafrika:(Nigeria,Gabon na Afrika Kusini). Suala la 'kuingilia Libya kwa kigezo cha kulinda raia' mapema likaanza kukiuka mamlaka ya Umoja wa Mataifa ya kulinda raia,na kuwa na lengo ya kuondoa utawala uliokuwa madarakani tena kwa vurugu nyingi zilizopelekea wengi kudhuriwa.Kutojali kulikoooneshwa na nchi za NATO kwa Umoja wa Afrika na PSC kumepita na kuendelea kukaliwa kimya.


Kisha madhara makubwa ya vita vya NATO nchini Libya,ukanda wa Sahel umeshuhudia migogoro kadhaa, mingi ikitokana na kuibuka kwa aina fulani ya makundi yenye silaha, uharamia na magendo. Kwa kisingizio cha migogoro hii, ambayo ilikolezwa na vita vya NATO, Ufaransa na Marekani ziliingilia kijeshi eneo la Sahel.

Mwaka 2014, Ufaransa **iliunda** G-5 Sahel, mpango wa kijeshi unaozihusisha Burkina Faso,Chad,Mali ,Mauritania na Nigern na kutanua ama kufungua kambi mpya ya kijeshi Gao,Mali; N'djamena, Chad; Niamey,Niger; na Ouagadougou,Burkina Faso. Marekani kwa sehemu yake **ilijenga** kambi nyingi za ndege zisizo na rubani huko Agadez, Niger ambapo kutokea huko imeendesha mashambulio ya ndege zisizo na rubani na upelelezi wa anga katika eneo la Sahel na jangwa Sahara.Hii ni moja kati ya kambi nyingi za Marekani barani Afrika. Marekani ina kambi za kijeshi zinazofahamika ishirini na tisa katika nchi kumi na tano barani Afrika, wakati Ufaransa ina kambi za kijeshi katika nchi 10 za Afrika. Hakuna nchi nyingine ambayo ina kambi nyingi za kijeshi kiasi hiki ndani ya Afrika.

Idadi ya kambi za kijeshi za kigeni katika Afrika ililishtua baraza la usalama na amani PSC, ambalo **lililiibua** suala hili kuwa suala maalum katika mkutano wake wa Mei 2016: Baraza lilionesha kuguswa na uwepo wa kambi za kijeshi za kigeni na ujenzi wa kambi mpya katika baadhi ya mataifa ya Afrika, kulikoambatana na suala la uwezo mdogo wa mataifa husika katika kudhibiti usambazaji wa silaha hizi kuingia na kutoka katika kambi za majeshi ya kigeni.Kwa minajiri hiyo, baraza lilitoa wito wa haja

ya nchi wanachama kuwa makini kila mara zinapoingia makubaliano ambayo yatapelekea uanzishwaji wa kambi za kigeni katika nchi zao.

Tangu mwaka 2016, kuna mabadiliko machache mno katika kuyafanyia kazi mapendekezo ya PSC. Inasemwa kuwa PSC haikutoa orodha ya nchi za kigeni zenye idadi kubwa ya kambi za kijeshi hapa barani, kwa kuwa suala la idadi linaashiria uhodari katika kuangamiza uhuru wa Afrika.Kama PSC lingezitaja Marekani na Ufaransa kuwa ndizo nchi vinara wa kuwa na kambi za kijeshi hapa Afrika,lingebainisha sababu mahususi ya ni kwanini Marekani na Ufaransa zinaendelea kuhitaji kuwa na uwepo wao kijeshi hapa Afrika.



**Arba Minch, Ethiopia** 6.040864 | 37.588118

Chanzo: Google Maps

Ni muhimu kutambua kuwa kuendelea huku kwa uwepo wa kambi za kigeni si desturi ya historia ya Afrika ya sasa wala si kwamba hakuwezi kubadilika. Mwaka 1965, Rais wa zamani wa Ghana Kwame Nkrumah alichapisha kitabu muhimu kiitwacho, *Ukoloni-mamboleo:Ngazi ya Mwisho ya Ubeberu (Neo-Colonialism: The Last Stage of*

*Imperialism),*kilichoakisi dhana ya kambi za kijeshi za kigeni.Haya yalikuwa ya kawaida nyakati za ukoloni mkongwe, ambapo kulikuwa na kambi kila sehemu ya bara hili kuanzia na kambi ya Uingereza kule Salisbury Rhodesia ya zamani(leo Harare, Zimbabwe) mpaka kambi ya Ufaransa kule Mers El Kébir, Algeria.Uingereza na Marekani zote zina kambi za kijeshi nchini Libya,tangu kambi ya jeshi la anga ya Wheelus mpaka kambi ya kijeshi kule Tobruk na El Adem. Kama malipo kwa ardhi na wanajeshi wanaowekwa katika kambi hizi, Marekani na Uingereza zinaipa Libya 'msaada' ,ambao Nkrumah aliuita 'malipo ya kupoteza uhuru'.

Hii hapa ni **tafakari na maoni** ya Nkrumah juu ya kambi za kijeshi ndani ya Afrika:

Taifa lenye nguvu duniani,madhali limeamua kwa minajiri ya mkakati wake wa ulimwengu kuwa ni lazima kwake kuwa na kambi ya kijeshi nchi fulani huru, ni lazima lihakikishe nchi ile ambayo kambi itawekwa iwe rafiki.Hii ni namna nyingine ya kuigawa Afrika(Balkanization).Kama kambi ya kijeshi itawekwa katika nchi ambayo ni dhalili kiuchumi kiasi haijimudu pasi 'msaada' kutoka katika taifa lenye nguvu kijeshi linaloimiliki kambi katika nchi ile dhalili, basi inaweza kusemwa kuwa ,usalama wa kambi ile utakuwa wa uhakika.Kama ilivyo kwa dhahania nyingi ambazo ukoloni-mamboleo unajikita kwazo,hii si sahihi. Uwepo wa wa kambi za kigeni unaamsha hasira ya watu dhidi ya mipango ya ukoloni-mamboleo kwa haraka na hakika kuliko kitu kingine, na katika Afrika

nzima kambi hizi zitapotea.Libya inaweza kuwa kielelezo kizuri juu ya namna sera hizi zilivyoshindwa.

Mwaka 1964, Gamal Abdel Nasser wa Misri aliamuru kuondolewa kambi hizi, na mwaka 1970-baada ya Kanali Muammar Gaddafi kuung’oa utawala wa kifalme- kambi ziliondolewa.

Miaka mitano kabla ya haya, Nkrumah kwa usahihi aliiona hali ya watu wa Libya.Hali hiyo kutoka mwaka 1965 ipo mpaka leo. Tangu ilipoundwa mwaka 2007, Kamandi ya Afrika ya Jeshi la Marekani (AFRICOM) ya serikali ya Marekani haijawahi kupata makaazi ndani ya bara la Afrika;makao makuu ya AFRICOM yapo Stuttgart,Ujerumani. Waafrika wanaendelea kuzipa msukosuko serikali zisijisalimishe kwa matakwa ya Marekani ya kuhamishia makao makuu ya AFRICAN kutoka Ulaya kuja AFRICA.

Nkrumah aliandika,ukoloni-mamboleo utakusudia kuigawa Afrika, kudhoofisha taasisi za dola za Afrika,kuzuia Umoja wa Afrika na uhuru, na hivyo kupenyeza mamlaka yake ili kutweza matumaini ya bara hili ya kuimarisha Umajumui wa Afrika. Si Jumuiya ya Nchi Huru za Afrika 1963-2002) wala Umoja wa Afrika (kuanzia mwaka 2002) ulioweza kutekeleza misingi mikuu miwili ya Umajumui wa Afrika:umoja wa kisiasa(political independence) na uhuru wa nchi(territorial sovereignty). Kuendelea kuwepo kwa kambi za majeshi ya kigeni haioneshi tu kutokuwepo umoja

na uhuru baina yetu; bali kunaruhusu kumegwa vipande na kutwezwa zaidi kwa watu na serikali za bara hili.



**Nzara, South Sudan** 4.634998 | 28.26727

Chanzo: Google Maps

# Kusalimisha Uhuru Wetu

Mwaka 2018, Wizara ya Ulinzi ya Marekani ilipendekeza kuwa Marekani na Ghana zikubaliane kuwa  na makubaliano ya kijeshi iliyoyaita Status of

Forces Agreement(SOFA),mkataba wa dola milioni 20 ambao utaliruhusu jeshi Marekani kutanua shughuli zake nchini Ghana. Mwezi March,kusambaa kwa kasi kwa taarifa za kutoridhishwa na makubaliano haya **kuliifanya** sehemu kubwa ya jamii kuingia mitaani kwa maandamano; vyama pinzani waliohofia juu ya uwezekano kuwa Marekani ingejenga kambi nyingine ya kijeshi nchini humo, waliibua hoja zao za kupinga suala hilo bungeni.


Kufikia April, Rais wa Ghana Nana Akufo-Addo alisema kuwa 'serikali yake haikuwa imetoa na haitotoa ridhaa ya kujengwa kambi ya kijeshi kwa Marekani'.Ubalozi wa Marekani Accra ulireajea tena kauli hii,na **kusema** kuwa 'Marekani haijaomba, na haina mpango wa kuanzisha kambi ya kijeshi nchini Ghana'.**Makubaliano** ya SOFA yalisainiwa mwezi Mei 2018.

Haihitaji kusoma kiundani waraka wa makubaliano kujua kuwa upo uwezekano wa Marekani kujenga kambi nchini. Kwa mfano,kifungu cha 5 kinaeleza,

Ghana inatoa ruhusa kutoingiliwa juu ya matumizi ya rasilimali-majengo tuliyokubaliana na eneo lake kwa majeshi ya Marekani,wakandarasi wake na wengine kama ilivyoridhiwa na pande zote.Rasilimali-majengo hayo yaliyokubaliwa na maeneo yake,ama sehemu yake hiyo iliyotolewa na Ghana itatumika kwa matumizi na majeshi ya Marekani kipekee ama kwa

pamoja na Ghana.Ghana itatoa haki,nafasi na matumizi ya njia ya kurukia ndege inayokidhi mahitaji ya Marekani.

Kupitia kifungu hiki,Marekani iliruhusiwa kuunda kituo chake ya kijeshi ndani ya Ghana.Kwa tafsiri yeyote, hii ina maana Marekani inaweza kuanzisha kambi ya kijeshi.Kusalimisha uhuru wa Ghana kunakuja nuruni ambapo makubaliano ya SOFA yanasema katika (kifungu cha 6) kwamba Marekani 'itapewa kipaumbele katika haki ya matumizi ya kituo kilichokubaliwa na maeneo yake' na hivyo haki ya matumizi kwa wengine 'yanawezekana kwa ridhaa ya majeshi ya Ghana na Marekani tu'.



**Ouagadougou, Burkina Faso** 12.361688 | -1.511828

Chanzo: Google Maps

Zaidi kifungu cha 3, kinasema kwamba wanajeshi wa Marekani 'wanaruhusiwa kubeba na silaha ndani ya Ghana wakiwa katika majukumu ya rasmi' na wanajeshi wa Marekani watapewa 'heshima na kinga sawa na wale waliokuwa katika majukumu ya kiutawala na maofisa

walio katika ujumbe wa kidiplomasia'.Kwa maneno mengine, wanajeshi wa Marekani wanaweza kupewa silaha na ikiwa watatuhumiwa kwa uhalifu, hawashitakiwa katika mahakama za Ghana.

Mwezi Machi 2018, waziri wa ulinzi, Dominic Nitiwul , alipewa changamoto katika redio na Kwesi Pratt wa Jukwaa la Wajamaa Ghana(SFG). Nitiwul alisema hakukuwa na chochote cha kipekee kuhusu makubaliano , kwa kuwa nchi nyingine za kiafrika-mfano Senegal-ilisaini makubaliano kama hayo. Nitiwul alisema,Ghana ilisaini makubaliano ya aina hiyo na Marekani mwaka 1998 na 2007, lakini hayo yalifanyika katika siri kwa kuwa hakukuwa na msamaha wa kodi**.** Pratt alionya kuwa Ghana 'itausalimisha uhuru wake' kama itaingia katika makubaliano haya.Maoni ya jumla ya wengi katika nchi yalipinga uwepo wa kambi, na ndio sababu serikali ya Ghana na Marekani zilikana juu ya kuwa kambi itajengwa.

Pratt alikuwa sahihi. Uwepo wa Marekani katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kotoka, Accra uligeuka kuwa moyo wa shughuli za mtandao wa mipango za jeshi la Marekani kwa Afrika Magharibi. Mpaka 2018, ndege za kila wiki kutoka kambi ya anga ya Ramstein Ujerumani zilitua Accra kwaajili ya ugavi wa masuala mbalimbali (ikiwamo silaha) kwaajili ya wanajeshi wa vikosi maalum wa Marekani takribani 1,800 waliopo maeneo mbalimbali Afrika Magharibi. Brigadia Jenerali Leonard Kosinski **alisema** mwaka 2019 kuwa ndege hizi za kila wiki zilikuwa ni 'kama ziara za basi tu'. Katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kotoka, Marekani ina eneo maalum la ulinzi wa ushirikiano.Hii ni kambi ya kijeshi kasoro jina.

# Nyayo za Marekani

Bara la Afrika si pekee lenye kambi nyingi a majeshi ya kigeni isivyo kawaida. Hili lipo ulimwengu mzima, kuanzia kambi za kijeshi za Marekani nchini Japan mpaka zile za jeshi la Uingereza nchini Australia. Hakuna jeshi lenye alama kubwa za **nyayo za kijeshi** katika ulimwengu kushinda Maerkani.Kwa kadiri ya Mpango wa Oparesheni Biashara wa Ulinzi wa Taifa wa Marekani (2018-2022),Jeshi la Marekani **linasimamia** 'mali zipatazo 568,000(zilizo katika mtindo wa majengo na vituo),ambavyo vipo katika maeneo 4800 hapa duniani kote'.

Mwaka 2019, AFRICOM waliunda **orodha** ya baadhi ya kambi zake zinazofahamika katika bara la afrika, walitofautisha kati ya zile zenya 'alama za unyayo zitakazosalia'(kambi ya kudumu) na zile zenye 'alama za unyayo zisizosalia' (kambi za muda):

| Kambi ya kudumu | Kambi za Muda |
| --- | --- |
| 1. Chebelley, Djibouti | 1. Bizerte, Tunisia |

| | |
|---|---|
| 2. Camp Lemonnier, Djibouti | 2. Arlit, Niger |
| 3. Entebbe, Uganda | 3. Dirkou, Niger |
| 4. Mombasa, Kenya | 4. Diffa, Niger |
| 5. Manda Bay, Kenya | 5. Ouallam, Niger |
| 6. Libreville, Gabon | 6. Bamako, Mali |
| 7. St. Helena, Ascension Island | 7. Garoua, Cameroon |
| 8. Accra, Ghana | 8. Maroua, Cameroon |
| 9. Ouagadougou, Burkina Faso | 9. Misrata, Libya |
| 10. Dakar, Senegal | 10. Tripoli, Libya |
| 11. Agadez, Niger | 11. Baledogle, Somalia |
| 12. Niamey, Niger | 12. Bosaso, Somalia |

13. N’Djamena, Chad

13. Galkayo, Somalia

14. Kismayo, Somalia

15. Mogadishu, Somalia

16. Wajir, Kenya

17. Kotoka, Ghana

Orodha hii haihusishi kambi ambazo Marekani inatumia ‘Majengo ya nchi mwenyeji’, kama vile kule Singo,Uganda na Theis,Senegal.

Uwepo wa kiasi kikubwa wa Majeshi ya Marekani katika bara la Afrika si jambo la kushangaza.Marekani ina jeshi kubwa na lenye nguvu duniani,kwa namna zote ikiwamo nambari kubwa ya vifaa vinavyowekwa na Marekani katika majeshi yake kupitia kambi zake pia majeshi yake ya maji na anga.Hakuna jeshi lingine duniani lenye kulingana na lile la Marekani, ambayo inatumia katika jeshi lake bajeti kubwa **zaidi** ya bajeti za kijeshi za nchi 11 zinazoifuatia ukizichanganya pamoja. China, ambayo inaifuatia Marekani katika matumizi kwenye sekta ya kijeshi

inatumia moja ya tatu ⅓ ya kiasi kinachotumiwa na Marekani kwa mwaka.

Alama za unyayo za jeshi la Marekani katika bara la Afrika si tu kubwa kwa kiasi kushinda kambi za nchi yeyote isiyokuwa ya kiafrika hapa barani,bali skeli kubwa ya uwepo wa shughuli za kijeshi unaipa sifa/tabia za tofauti kiubora;sifa hizi zinajumuisha uwezo wa Marekani kulinda maslahi yake ndani ya bara na kujaribu kuzuia ushindani katika udhibiti wake wa rasilimali na masoko. Kuna majukumu mawili ambayo yanatekelezwa na na jeshi la Marekani barani Afrika:


1. **Kazi ya Upolisi.** Jeshi la Marekani linafanya kazi si tu kwaajili ya kutoa manufaa ya Marekani na tabaka lake tawala la wachache ,lakini linafanya kazi-sambamba na majeshi ya mataifa ya Umoja wa Kujihami wa Nchi za Magharibi(NATO), ikiwamo Ufaransa - kama muhakikishaji/mlinzi wa maslahi ya makampuni makubwa ya wamagharibi na misingi ya ubepari.Nkrumah alifikia hitimisho kama hilo mwaka 1965,alisema malighafi za 'Afrika' ni muhimu mno kwa uimarishaji wa mataifa ya NATO.Viwanda vyao,hususani vya kimkakati na vya nyuklia, vinategemea mno malighafi zitokazo katika nchi ambazo hazijapiga hatua kubwa kimaendeleo. Taarifa kutoka jeshi la Marekani zinaonesha kuwa mara kwa mara wajibu wa majeshi yake ni katika kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali kwa makampuni makubwa-hususani nishati -na kuendelea kudhibiti mielekeo ya bidhaa katika mikondo ya usafiri wa mali. Ripoti hizo

zinajumuisha ***Sera ya Taifa ya Nishati***(May 2001) kutoka National Energy Policy Development Group iliyokuwa ikiongozwa na Makamo wa Rais wa zamani Dick Cheney na ***Ukaguzi na Uimarishaji wa Sekta ya Uzalishaji na Ulinzi na Uimarishaji wa Mnyororo wa Ugavi wa Marekani***(September 2018) kutoka Interagency Task Force katika kutekeleza amri ya Rais namba 13806. Katika hali hii,jeshi la Marekani-sambamba na washirika wa NATO-wanafanya shughuli kama upolisi si kwaajili ya jumuiya ya ulimwengu, isipokuwa kwa maslahi ya ubepari**.** Sambamba na Marekani ni Ufaransa, ambayo uwepo wake kijeshi nchini Niger umeungana kwa ukaribu na umuhimu na ya sekta ya nishati ya Ufaransa, ambayo inahitaji Urani inayochimbwa Arlit(Niger). Taa moja ya umeme kati ya tatu za ufaransa inawaka kutokana na nishati kutoka katika mji huu huko Niger, ambao **umefanywa kama kambi ya jeshi** na majeshi ya Ufaransa.

2. **Vita baridi mpya.** Kadiri ambavyo maslahi ya kibiashara ya sekta ya umma ama binafsi ya China yanavyoongezeka katika bara la Afrika, huku kampuni za China zikiendelea **kuzipiku** kampuni za kimagharibi, jiatihada za Marekani kuimeza China umeongezeka. ***Mkakati Mpya kwa Afrika*** wa serikali ya Marekani(2019) unatoa taswira juu ya hali katika vigezo vya ushindani: 'Washindani wakubwa wenye nguvu, waitwao China na Urusi, wanatanua kwa haraka ushawishi wao wa kifedha na kisiasa maeneo mengi ya

Afrika.Wanalenga kwa makusudi na nguvu uwekezaji wao katika ukanda huu ili kupata manufaa ya kiushindani dhidi ya Marekani'. Umoja wa Ulaya ulifuatia kutoa **ripoti** iliyoitwa *Kuelekea Mkakati Uliosheheni na Afrika* (2020), ambao-licha ya kuwa hauitaji China wazi wazi- unaonesha hofu kuhusu 'ushindani kwenye rasilimali asili'.

Hoja hizi mbili-za upolisi na vita baridi mpya-zinahitaji ufafanuzi zaidi**.**



**Agadez, Niger** 16.950278 | 8.013889

Chanzo: Google Maps

## Unyonyaji Rasilimali


Afrika ni eneo la pili kwa ukubwa wa eneo la ardhi hapa duniani ikiwa ni bara la **pili kwa ukubwa** wa idadi ya watu(watu bilioni 1.34 mwaka 2020 )-zaidi ya idadi ya watu wa bara la Marekani ya Kaskazini na Ulaya wakijumlishwa pamoja(watu bilioni 1.1).Asia ndilo bara kubwa lenye idadi kubwa ya watu(watu bilioni 4.64).

Ardhi ya Afrika inakusanya idadi muhimu ya rasilimali asili: 98% ya chromium yote duniani, 90% ya cobalt yote duniani, 90% ya platinum yote duniani, 70% ya coltan yote duniani, 70% ya tantalite yote duniani, 64% ya ya manganizi, 50% ya dhahabu, na 33% ya urani, sambamba na kiasi kikubwa cha akiba ya madini mfano bauxite, almasi, tantalum, tungsten,na bati. Bara hili lina 30% ya hazina yote ya madini yote , 12% ya hazina yote ya mafuta inayotambulika, 8% ya gesi asilia, na 65% ya ardhi inayofaa kwa shughuli za uzalishaji chakula na mifugo.

Programu ya mazingira ya Umoja wa Mataifa **inakadiria** kuwa mtaji asili wa Afrika(natural capital) ni unachangia kati ya 30%-50% ya ukwasi wa nchi za Afrika. Mwaka 2012,Umoja wa Mataifa ulikadiria kuwa rasilimali asili zilichangia 77% ya bidhaa zilizosafirishwa nje na 42% ya mapato ya serikali za Afrika.

Utegemezi wa dola za Afrika katika uuzaji nje wa malighafi za aina tofauti-kwasababu ya makampuni makubwa ya kimataifa na kutokuwepo kwa viwanda katika nchi nyingi za Afrika-kumeziweka katika nafasi ya

utegemezi kwa mtaji unaotoka nje. Hali ya utegemezi iliundwa na sera za watawala wa kikoloni ,ambao bado waliendeleza, shughuli za kiuchumi katika Afrika kwa msingi wa kuvuna malighafi ambazo ziliuzwa kwa mtindo wa upendeleo wa wakoloni kwa watawala wa nchi zao.Utegemezi huu ulirithiwa na vizazi vya watawala wetu ambao uliwapatia faida wao na hawakujishughulisha kuubadili muundo wake. Hivyo dola za Afrika zinategemea mapato kutoka nje kwa kuuza malighafi,programu za misaada kutoka nchi za magharibi na katika misaada ya kitaasisi.



**Entebbe CSL, Uganda** 0.046175 | 32.45588

Chanzo: Google Maps

Utegemezi wa namna hiyo unatengeneza njia zisizoruhusiwa za kilaghai toka kwa serikali hizi za nje ambazo zina maslahi ya kudumu katika Afrika. Serikali zinazotawala zinahonga rasilimali asili kulinda misaada kutoka kwa washirika wa nje pasi kuzingatia sana mahitaji na masharti ya misaada. Masharti ya misaada hii yananyonya mapato stahiki.Mfano,Kamisheni ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwaajili ya Afrika **inaripoti** kwamba kwa miaka hamsini iliyopita ,mikondo ya fedha iliyo haramu imepelekea upotevu wa takribani dola za Marekani trillioni moja(1$ trillion), 'kiasi ambacho karibu kiko sawa na gharama zote za misaada ya kimaendeleo katika kipindi hicho hicho'.

Fedha hizi adhimu zingeweza kuunda uchumi-mseto(diversified) wa nchi mbalimbali, kujenga miundombinu inayokosekana, na kunawirisha mapato jamii(social wages) hapa barani. Utegemezi wa kiuchumi unaminya nafasi za machaguo kwa serikali za Afrika, ambazo zinaendelea kuwa watwana kwa maslahi na mamlaka za nje. Miongoni mwa serikali zizofanywa watwana, utashi wa kisiasa kupinga uingiliwaji kijeshi -toka kuanzisha kambi za kigeni mpaka kuruhu majeshi ya kigeni kufanya shughuli zao kwa njia maelfu-hauwezi kuwepo.

Makundi mbalimbali ya umajumui wa Afrika yameibuka katika muongo uliopita kupinga utegemezi huu, ikiwemo mbadala kwa Afrika dhidi ya Programu ya Ulegezaji Masharti ili kurejesha mageuzi ya kiuchumi na kijamii(1989),Dira(***Vision***) ya Madini ya Afrika(2008), Azimio la Gaborone la Maendeleo Endelevu Afrika(2012), Azimio la Arusha la mkakati wa maendeleo endelevu wa Afrika baada ya Rio+20 (2012), Jukwaa la maendelo ya Afrika katika (2014), mkutano wake wa nane,na kufikia kilele cha kuasiliwa na AU kwa mpango wa utekelezaji wa miaka kumi ya mwanzo(2014-2023),kuorodheshwa katika waraka wa tatu wa *Agenda 2063:Afrika Tuitakayo (2015).* Nyaraka hizi zote-kwa ngazi mbalimbali za msisitizo- zinaonesha umuhimu wa kuvunja utegemezi wa usafirishaji malighafi, usimamizi bora wa mikataba inayoingiwa na makampuni makubwa, na kutumia mapato yatokanayo na na mauzo ya nje katika kuboresha maisha ya kijamii kama inavyoanishwa katika makubaliano ya Umoja wa Mataifa juu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Kushindwa kutumia rasilimali kwa tija na kuendesha programu zinazotoa kipaumbele kwa maendeleo ya watu kunazalisha muktadha wa migogoro ya kisiasa na kijeshi, ikiwamo makundi ya uvamizi ambayo mara nyingi hujiunda katika minajiri ya kidini na kikabila na kutanuka kwa suala la uhamiajia barani kuelekea Ulaya. Matokeo haya mawili ya matatizo ya kina ya kiuchumi katika dola za kiafrika-migogoro na uhamiaji-yanazalisha

kisingizio kwa nchi kama Marekani na Ufaransa kuanzisha kambi za kijeshi barani Afrika.

- **Migogoro**. Serikali ya Marekani imeanzisha mahusiano ya kawaida ya kijeshi-ikiwamo kambi za muda mfupi(lily pad bases)-nchini São Tomé na Príncipe katika Ghuba ya Guinea. Kwa upande mwingine, ufafanuzi kwa uwepo wa Marekani kwa eneo hilo hauachi kutaja kuwa jambo hili ni kwasababu ya kulinda mafuta(shughuli za uchimbaji na uchukuzi) kuelekea Marekani; Nigeria ni mwanachama wa Jumuiya ya Mataifa Wazalishaji Petrol (OPEC), ni mzalishaji mkubwa nambari 11 wa mafuta ulimwenguni. Kwa upande mwingine Marekani inasema uwepo wake kijeshi katika Ghuba ya Guinea una lengo la kudhibiti kukua kwa makundi ya silaha ya kiislamu, hususani ISIS na Al Qaeda, japokuwa maofisa wa serikali wanakubali ya kuwa makundi hayo hayana uwepo ambao ni tishio kwa eneo hilo.

Katika Afrika ya Kati, AFRICOM imekuwa ikijihusisha kwa miongo kadhaa na kutoa mafunzo kwa jeshi la Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo(DRC), hususan katika kambi, kambi ya kijeshi nje kidogo ya Kisangani. **Taarifa** ya AFRICOM mwaka 2010 ,mafunzo ya kijeshi ni jambo yatakuwa 'sehemu ya jambo la muda mrefu katika mahusiano baina ya Maerkani na DRC ili kukuza mageuzi ya sekta ya usalama. Nchini DRC, ambayo itaisaidia serikali ya DRC katika jitihada zake kuliimarisha jeshi lake'. Mahusiano haya baina ya DRC na AFRICOM yameendelea kukua tangu kipindi hicho.

Ugunduzi mkubwa wa mafuta (**ilikadiriwa** mapipa bilioni 1.7) ulifanywa katika eneo la mpaka kati ya DRC na Uganda katika ukanda wa ziwa Albert mwaka 2007. Kwa hiyo haishangazi. Hata hivyo shughuli za kijeshi zimeongezeka ukanda huu. Hii inashuhudiwa waziwazi katika mji wa Beni, Kivu ya Kaskazini. Beni ni kitovu cha mauaji mengi ya kikatili mara nyingi yakihusishwa na kundi la waasi la nchini Uganda liitwalo Allied Democratic Front(ADF), ambalo linafanya shughuli zake Kongo DRC tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990. Juni 27,2021, ujumbe wa maofisa wa AFRICOM ulifika DRC **kujadili** na jeshi la Kongo juu ya hitaji ya 'mashirikiano, usalama na jitihada za utengemavu na kufanya kazi pamoja kukuza weledi wa jeshi la DRC na kuimarisha zaidi ushirikiano'.

Machi 10, 2021 Wizara ya dola ya Marekani(US State Department) **iliitaja/kuipa hadhi** ADF kuwa 'kikundi cha kigaidi cha nje' na 'kikundi cha kigaidi cha ulimwengu' ingawa taasisi wenyeji na kundi la wataalamu wa Umoja wa Mataifa juu ya DRC linasema hakuna ushahidi unaiunganisha ADF na ISIS. Wizara ya dola ya Marekani ilichukua msimamo huu kutokana na **madai** yaliyotolewa na Taasisi ya Bridgeway, taasisi ya matendo ya huruma (charity organization) iliyo tawi la kampuni ya Bridgeway Capital Manangement ya huko Texas.

Utambuzi huu unairuhusu Marekani kuongeza uwepo na shughuli zake za kijeshi nchini DRC.

Eneo mahususi kwa uwepo huu ni lile lililo karibu na hifadhi/hazina ya mafuta. Jeshi la Marekani pia litaendelea kuhakikisha utangamano wa viongozi wababe wa kiafrika, ambao wataendelea kutegemea usaidizi wa Marekani katika kusalia kwao zaidi madarakani.

- **Uhamiaji.**Programu zilizosukumwa na ushauri wa IMF na kushindwa kwa dola za Afrika kusimamia mauzo ya rasilimali katika namna ambayo ingetoa ahueni kwa watu kumepelekea wimbi kubwa la wahamiaji maeneo mbalimbali ya nchi.Robo ya takribani wahamiaji milioni 41.3 waliotawanyika kutokana na vurugu na migogoro walijaribu kuelekea Ulaya wakati wengine wakielekea maeneo mengine mbalimbali ya Afrika.

  Wahamiaji hawa ambao wanakusudia kwenda Ulaya husafiri kuvuka jangwa la Sahara mpaka Libya, iliyovunjwa vunjwa na vita vya NATO, na kisha kuvuka bahari ya Mediterrania. Safari hatari, lakini Umoja wa Mataifa ulipofanya utafiti, wale wanaofanikiwa kuvuka jangwa na bahari, 90% ya wahamiaji walisema wangerudia tena ikiwa wangejikuta wapo Afrika.

  Majaribio ya Ulaya kuzuia wahamiaji katika bahari ya Mediterrania yamekuwa hayana mafanikio. Majeshi ya kigeni yamekuwa yakitumika Sahel kudhibiti uhamiaji na kuwasogeza wahamiaji mbali iwezekanavyo kutoka mipaka ya Ulaya. Hii ndio kwa sehemu sababu alianzisha suala la G5 Sahel Initiative na ni sababu kwanini

Marekani walijenga kambi kubwa kabisa ya ndege zisizo na rubani huko Agadez, ambayo zinatoa taarifa muhimu za upelelezi wa anga juu ya wahamiaji katika ukanda ule. Yafanyacho mataifa ya Ulaya ni sawa na kusema wamesogeza mipaka ya nchi zao mbali mno na kwao na kuhakikisha kuwa makabiliano baina yao na wakimbizi na wahamiaji yanafanyika mbali kabisa nje ya uwepo wa vyombo vyao vya habari. Hii ni aina ya kutoa kandarasi kwa mtu mwingine(outsourcing) ya kushughulikia janga la la wakimbizi: Wamagharibi wanaendesha sera ya mbaya ya kinyume na wahamiaji wakati huohuo wanajiweka kutokuwa na hatia wakati wafuasi wake wakiendelea kutenda kazi chafu.Ulaya imehamisha mipaka yake ya kusini kutoka katika ncha ya kaskazini ya bahari ya Mediterrania mpaka eneo la kusini la jangwa la Sahara, sasa likiwa limetawaliwa na kambi za kijeshi toka Mauritania mpaka Chad.


Hoja ya kuzuia migogoro na udhibiti wa wahamiaji inafahamika. Lakini, mara moja moja, nia ya ndani hufafanuliwa na baadhi ya maofisa wa Marekani. Kama Commodore John Nowell, anayeendesha kituo cha ushirika cha AFRICOM cha Afrika, mwaka 2008 **aliyesema**, 'Tusingekuwa hapa kama si maslahi ya Marekani' , kwa kusema 'hapa', Commodore Nowell alimaanisha Barani Afrika.

# Vita baridi mpya

Katika *mapitio ya ripoti ya ulinzi ya miaka minne* ya serikali ya Marekani mwaka 2006,waandishi **waliandika** kuwa, ‘kama kuna mataifa miongoni mwa yaliyo na nguvu na yanayoibukia, China ina uwezo mkubwa kushinda taifa lolote kuikabili Marekani na kuweka teknolojia za kijeshi haribifu ambazo baada ya kipindi fulani zitayapiku manufaa yaliyozoeleka ya Marekani’. Kimsingi,kwa kiasi kikubwa uwezo mkubwa wa uchina ni wa kujilinda, kwa kuwa uchina imejenga uwazo wake wa kijeshi kwaajili ya kuzilinda fukwe zake na eneo la bara.

Waziri wa masuala ya kigeni wa China Wang Yi **amesisitiza** kuwa nchi yake imechukua wajibu katika ushirikiano wa wengi(multilateralism): ‘Uchina haijawahi kuusaka uongozi wa ulimwengu’, aliyasema hayo siku ya tarehe 24 AprilI,2021. Wanachokionesha wana mipango wa Marekani ni kuwa wasingependa kuona mafanikio  ya China katika biashara na kisiasa yanayotoa changamoto kwa utawala wa ulimwengu wa Marekani.

Kama ambavyo Commodore Nowell aliweka vema, maslahi ya Marekani ndio sababu ya uwepo wao kwenye ukanda waliokuwepo; hatari yeyote kwa maslahi yao lazima izuiwe kwa namna yeyote.



**Kambi ya Lemonnier, Djibouti** 11.544409 | 43.14707

Chanzo: Google Maps

Mwaka 2013, serikali ya China ilizindua mradi mkubwa uitwao Belt and Road Initiative (BRI). Kabla ya kurasimishwa kwa BRI, jukwaa la mashirikiano baina ya Afrika na China liliundwa mwaka 2000 na, mwanzo, nchi arobaini na nne (44) za kiafrika(nchi hamsini na tatu kati ya hamsini na tano barani Afrika zimeanzisha mahusiano na China kupitia jukwaa

tangu kipindi hicho).Tangu mwaka 2013,China imewekeza katika takribani nchi zote za Afrika, ambapo zote isipokuwa Eswatini(zamani ikiitwa Swaziland) zimevunja mahusiano na Taiwan na kuitambua Jamhuri ya Watu wa China.

Kwa miaka mingi China imesaini makubaliano ya ushirikiano na umoja wa Afrika(AU), ikiwemo ya mwaka 2015 yaliyo ndani ya mizani ya Agenda 2063 kusaidia ujenzi wa miundombinu. China imewekeza kiasi kikubwa cha fedha kwenye miundombinu ya muhimu kama ujenzi wa reli kati ya Mali na Guinea na reli kutoka Sudan mpaka Senegal; katika miundombinu ya nishati, mfano bwawa la uzalishaji umeme wa maji la Mambilla litakalozalisha Megawatt 2600 nchini Nigeria na lile la Bui la nchini Ghana litakalozalisha Megawatt 400; na kwenye mawasiliano, mfano vifaa vya mawasiliano kwa nchi za Ethiopia, Ghana, Kenya, na Sudan. Desemba ya 2020, ujenzi wa makao makuu ya kituo cha kuzuia na udhibiti wa magonjwa cha Afrika(Africa Centres for Disease Control and Prevention) chenye thamani ya dola milioni 80 unaofadhiliwa na China **ulianza** kusini mwa Addis Ababa,Ethiopia.Mpaka sasa kuna miradi takribani 600 **iliyokamilika** iliyo chini ya mpango wa BRI kote ulimwenguni.

Msaada wa China-tofauti na msaada wa IMF, Uwekezaji wa kibiashara wa nchi za magharibi, na usaidizi wa maendeleo kwa nchi za nje-hauambatanishwi na masharti magumu ya kudhohofisha. Ushahidi wa masharti rahisi unajitokeza katika makubaliano mbalimbali yaliyosainiwa na China, lakini zaidi ya hayo, inatokana zaidi na nadharia ya China ya

**mtaji stahimilivu**(patient capital), ambayo hadi sasa imeasiliwa ndani ya mipaka ya China lakini taratibu-kupitia benki za serikali za China-China imeibuka na kuwa muwekezaji mkubwa nje ya mipaka yake. China kwa sasa ni nchi ya **pili kwa kwa uwekezaji mkubwa** ulimwenguni, huku benki ya China Export-Import Bank na China Development Bank wakiwa wawekezaji wakubwa. Mikopo ambayo wakala hawa wa serikali(benki tajwa hapo juu) huitoa ni uwekezaji wa muda mrefu na si haipangiwi muda mfupi kuilipa. China inaelewa vilivyo kuwa mikopo hii inatolewa kutafuta suluhi ya shida ya miundombinu hivyo kusaidia maendeleo ya jamii. Nchi mkopaji hupewa ahueni kwa kuwa faida hutabiriwa kuja baada ya kipindi kirefu. Mfano, 30% na 80% ya uwekezaji katia Asia ya kati na Pakistani haitarejeshwa.

Badala ya kuunda sera yake ya msaada ya kibiashara na maendeleo yenye taswira utu ambayo itawanufaisha watu wa Afrika, Marekani imaenzisha 'vita baridi mpya' dhidi ya China ndani ya bara la Afrika.Maendeleo/maboresho ya AFRICOM mwaka 2007 sambamba na kuzidishwa kwa kambi za kijeshi za Marekani na washirika wake katika ukanda wa Sahel, pembe ya Afrika, na kwingineko ni sehemu ya hii Vita Baridi Mpya.Kimsingi,Vita Baridi Mpya inaundwa katika vita vya upotoshaji taarifa, ambavyo vinabebwa na masuala mawili yafuatayo: '**Ukoloni' mpya wa Kichina.** La kushangaza, wakoloni wakongwe ambao wanaendeleza sera ya ukoloni mamboleo kwa Afrika na China-kama ilivyoonyeshwa na Nkrumah na ikithibiti katika muundo wa kambi-

sasa wanawageuzia kibao China na kuwatuhumu kuwa mamlaka ya kikoloni.Manneno makuu yanayotumika katika vita hivi vya upotoshaji taarifa ni madai kuwa China inatumia vyanzo vyake vya fedha kuyaingiza mataifa katika mtego wa madeni,ambao unazilazimisha nchi hizi kukabidhi rasilimali zao kwa gharama ndogo. Msemo 'diplomasia ya mtego wa madeni' inatumika dhidi ya China, japokuwa si China iliyolazimisha mikopo ya masharti ya ulegezaji uchumi ambayo ilizitupia nchi nyingi za Afrika katika mtego wa madeni yenye majanga ambayo yameongezeka katika kipindi cha janga la UVIKO-19. Haikuwa China, isipokuwa IMF, ambayo, ilileta muundo wa sera inayoendeshwa na Idara ya Hazina ya Marekani(US Treasury department). Wakati Marekani ikiishutumu China kwa kukataa kujadiliana tena masharti[ya mkopo], na kuchukua udhibiti wa muundombinu wenyewe', kiuhalisia ni kuwa wakopeshaji wa China wamefuta, wameahirisha, na wameunda upya masharti ya mikopo iliyopo(kabla na kipindi cha janga la UVIKO-19) na hawaja wahi kuzuia mali kutoka nchi yeyote. Maprofesa wawili wakongwe walichapisha makala katika The Atlantic mnamo February 2021 yenye kichwa cha habari kilichosema '"Mtego wa Mkopo" wa Kichina si halisia'. Shitaka kuhusu ukoloni dhidi ya China linaundwa na nchi ambazo zina historia iliyoandikwa vema mno kuhusu ukoloni na ukoloni-mamboleo katika Afrika.

- **Uwezo wa kijeshi wa China**. Mamlaka za ukoloni mkongwe zinaishutumu China kwa kuimarisha jeshi lake katika Afrika. Katika

kuhuisha hadaa ya, kamanda wa AFRICOM Jenerali Townsend hivi karibuni alitoa madai yasiyo na uthibitisho kwamba China inakusudia kujenga kambi ya jeshi la wana maji katika pwani ya Afrika Magharibi. Kimsingi, uwepo wa China kijeshi katika Afrika ni sawa na haupo ukilinganisha na alama za nyayo za kijeshi za nchi za Magharibi. Mwaka 2008, China iliunga mkono jitihada za kupambana na uharamia katika pembe ya Afrika na Ghuba ya Aden ; oparesheni hizi zilitokana na azimio namba 1816 (2008) la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ambapo nchi wanachama wa Umoja wa mataifa ziliomba Umoja wa Mataifa kuisaidia serikali ya mpito ya Somalia kwa 'namna zote iweze kupambana na uharamia na ujambazi wa kutumia silaha'. Baada ya muongo mmoja, China iliunda kambi yake ya kwanza ya kijeshi nje ya nchi, nchini Djibouti. Kazi za kambi hii zilikuwa aina mbili, kwanza kutoa usaidizi wa mipango kwa meli ilizokuwa zikisindikiza meli za mafuta na mizigo za China katika Ghuba ya Aden, na pili kusaidia kampeni ya kimataifa dhidi ya uharamia. Wakati huohuo, katika eneo lenye shughuli nyingi za kijeshi la pembe ya Afrika, serikali ya China inafadhili ujenzi wa reli ya umeme ya Ethiopia na Djibout kwa mradi wa dola bilioni 4, wakati benki ya China Export-Import Bank ikitoa fedha zaidi ya dola milioni 300 kwaajili ya ujenzi wa bomba la maji kuleta maji safi ya kunywa kutoka Ethiopia kwenda Djibouti.Utaratibu amani wa China ni tofauti mno na shughuli za kijeshi za mataifa ya Magharibi ambao umejikita katika katika upolisi na silaha wenyewe unachagua kujikita

katika maendeleo ya uchumi unaaongozwa na miundombinu na kuondoa umasikini.

## Umoja wa African

Mwaka 2016, Umoja wa Afrika(AU) uliibua suala la kambi za kijeshi za mataifa ya kigeni ndani ya bara la Afrika. Mjadala haujatanuka sana tokanyakati hizo.Hali ya utegemezi ya Umoja wa Afrika kirasilimali na ufadhili kutoka nje katika shughuli zake, ikiwamo shughuli za kulinda amani, umeminya uwezo wake kuchukua maamuzi huru, ya kimkakati na kimbinu katika utendaji wake wa kazi.Katika suala la kulinda amani, kwa mfano, mataifa ya Afrika yanachangia asilimia mbili tu (2%) tu ya gharama zashughuli za kulinda amani na usalama za AU, wakati wafadhili wa nje - kama vile Umoja wa Ulaya - **wakitoa** asilimia tisini na nane (98%) ya fedha. Hii imezuia mno uwezo wa Baraza la Amani na Usalama la AU kuendesha agenda zake na ndio sababu AU haijaweza kuendeleza mjadala juu ya kambi za kijeshi za kigeni barabara.

Siku ya Oktoba 15,2003, Nile Garddiner na James Carafano wa taasisi ya Heritage Foundation walichapisha **waraka maalumu** (white paper) ulioitwa *Usaidizi wa Kijeshi wa Marekani kwa Afrika:Suluhu Bora*. Humo walitoa hoja kuwa serikali ya Marekani iunde kamandi ya kijeshi ya Afrika ambayo itaingilia katika Afrika ‘wakati maslahi nyeti ya Marekani

yatapotishiwa’ kama ambavyo imefanya hivyo Marekani ya Ulatini na Karibian Marekani ilipounda Kamandi ya Kijeshi ya Kusini mwaka 1963. Hii iligeuka uhalisia mwaka 2007.Mataifa mawili ya Afrika, Botswana na Liberia, yalionesha yangependa kuikaribisha na kuweka makao makuu ya AFRICOM. Wakati huu Afrika Kusini ilipinga AFRICOM kuletwa hapa barani Africa.Kupitia kuingilia kati kwa AU, Botswana pamoja na Liberia zilirudisha nyuma azma yake.

Hali ya kuzuia makao makuu ya AFRICOM kuwekwa ndani ya Afrika imeendelea kusalia miongoni mwa watu wa Afrika. Hata hivyo,hiyo haikuzisimamisha jitihada za Marekani na baadhi ya wakuu wa dola wa kiafrika. Katika kikao na waziri wa masuala ya kigeni wa Marekani Blinken tarehe 27 April 2021, Rais wa Nigeria Muhammadu Buhari aliomba Marekani **ihamishe** makao makuu ya AFRICOM kutoka Stuttgart ,Ujerumani kuyaleta barani Afrika ili kukabiliana na vitendo vya uvamizi na mashambulio ya kigaidi.Kuongezeka kwa migandamizo kutoka katika makundi yenye msimamo mkali ya kiislamu na wapinzani wengine kumeondoa hali ya utulivu ndani ya Nigeria na huwend ahiyo ndio sababu ya maombi hayo ya Rais Buhari, ingawa hakupendekeza makao makuu ya AFRICOM yawe nchini kwake Nigeria. Msimamo wa Nigeria umebadilika sana kutoka kwenye msimamo wao wa awali ambao muongo uliopita ilikuwa ikipinga uwepo wa AFRICOM ndani ya Africa. Hata hivyo kambi za kijeshi za Marekani zimeendelea kuongezeka tangu wakati huo. AU ilionesha hatari ya ongezeko hilo mwaka 2016 lakini,hata wakati ule,jambo


ambalo ambao AU iliweza kulikusanya ni kauli tu zisizo na uzito: ‘hofu’ na ‘uthubutu hafifu’. Licha ya maneno haya, AFRICOM ilijipenyeza katika AU na kujishikiza katika Baraza la Amani na Usalama(PSC) na maofisa wa Divisheni ya Tahadhari na Kuzuia Migogoro ya AU, pamoja na Divisheni ya Kusaidia Shughuli za Amani.

Kuingia kwa AFRICOM katika AU kwa jina la ‘kufanya kazi pamoja’ kuunganisha walinda amani na majeshi ya Marekani, Marekani imeanza kuandaa mpango wa usalama wa AU moja kwa moja.

Katika kitabu chake cha Ukoloni-mamboleo katika Afrika, Nkrumah aliandika:

Hatari kwa amani ya ulimwengu haitokani na matendo ya wale wanaofanya jitihada kuumaliza ukoloni-mamboleo isipokuwa kwa kutofanya lolote kwa wale wanaoruhusu uendelee. Kama vita ya dunia haitopaswa kutokea basi itapaswa izuiwe kwa hatua chanya. Hatua chanya zimo ndani ya uwezo wa watu ambao kwa sasa wanateseka chini ya ukoloni-mamboleo lakini uko ndani ya uwezo wao kama watafanya hivyo mara moja(bila kuchelewa),katika makubaliano na umoja.

Maneno haya ya mwaka 1965 yanathibitisha ukweli leo.




**Kambi ya  Simba, Kenya** -2.171847 | 40.897016

Chanzo: Google Maps

## Rejea:

Campbell, Horace G. ‘The Quagmire of US Militarism in Africa’, *Africa Development* 45, no. 1 (2020): 73-116.

Charbonneau, Bruno. ‘De Serval à Barkhane: les problèmes de la guerre contre le terrorisme au Sahel’, *Les Temps Modernes* 2 (2017): 322-340.

de Montclos, Marc-Antoine Pérouse. ‘La politique de la France au Sahel: une vision militaire’, *Hérodote* 172, no.1 (2019): 137-152.

Enloe, Cynthia. *Bananas, Beaches and Bases: Making Feminist Sense of International Politics*. Berkeley: University of California Press, 1990.

Evrard, Camille. ‘Policier le désert. Ordre colonial, <<guerriers nomades>> et État postcolonial (Niger et Mauritanie, 1946-1963)’, *Vingtiéme Siècle. Revue d’Histoire* 4, no. 140, (2018): 15-28.

Gwatiwa, Tshepo, and Justin van der Merwe, eds. *Expanding US Military Command in Africa: Elites, Network, and Grand Strategy*. New York: Routledge, 2020.

Klin, Tomasz. ‘The Significance of Foreign Military Bases as Instruments of Spheres of Influence’, *Croatian International Relations Review* 26, no. 87 (2020): 120-144.

Lutz, Catherine, and Cynthia Enloe, eds. *The Bases of Empire: The Global Struggle against U.S. Military Posts*. New York: New York University Press, 2009.

Luzzani, Telma. *Territorios vigilados: Como opera la red de bases militares norteamericanas en Sudamérica*. Buenos Aires: Debate, 2012.

Nkrumah, Kwame. *Neo-colonialism: The Last Stage of Imperialism*. New York: International Publishers, 1965.

Sun, Degan, and Yahia Zoubir. ‘Sentry Box in the Backyard: Analysis of French Military Bases in Africa’, *Journal of Middle Eastern and Islamic Studies (in Asia)* 5, no. 3 (2011): 82-104.

Turse, Nick. ‘Pentagon’s Own Map of US Bases in Africa Contradictions Its Claim of “Light” Footprint’, *The Intercept*, 27 February 2020.

United States Government Accountability Office. *DOD Needs to Reassess Options for Permanent Location of US Africa Command: Report to Congressional Committee*. Washington, DC: GAO 13/646, 2013.

United States Africa Command Public Affairs Office. *Fact Sheet: United States Africa Command*. 15 April 2013.

Wang, Lei. ‘China and the United States in Africa. Competition or Cooperation?’, *China Quarterly of International Strategic Studies* 6, no. 1 (2020): 1–19.

Vine, David. ‘No Bases? Assessing the Impact of Social Movements Challenging US Foreign Military Bases’, *Current Anthropology* 60, no. S19 (February 2019): S158-S172.

Vine, David. *Base Nation: How U.S. Military Bases Abroad Harm America and the World*. New York: Metropolitan Books, 2015.

Yeo, Andrew. ‘The Politics of Overseas Military Bases.’ *Perspectives on Politics* 15, no. 1 (March 2017): 129-136.

Yeo, Andrew. *Activists, Alliances, and Anti-U.S. Base Protests*. New York: Cambridge University Press, 2011.